6/01/2021



The Guardian

l

m as

rced
:ause
their
vised
y got
ouncil
ablish
l send
" said

l as a
; there
at has
saying
s land
ues in
onflict
ists.
joying
ts SDC

eita, a
ecious
: times



**CCM secretary general Dr Bashiru Ally Kakurwa (3rd-L) accompanied is taken around a livestock farm in Karagwe District on Monday.** Photo: Correspondent Eliud Rwechungura

Scanned with CamScanner

Habari Leo, uk. 17 - 06/01/2021

# Ujenzi kiwanda cha kusindika maziwa waenda vyema

**Na Mwandishi Maalumu, Karagwe**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dk Bashiru Ally amekagua ujenzi wa kiwanda cha cha kusindika maziwa na vyakula vya mifugo cha Kahama Fresh Ltd kinachojegwa kata Kihanga, Karagwe mkoani Kagera.

Pia katika ziara hiyo alizuru shamba la mfano la mahindi na eneo la ufugaji wa ng'ombe, mbuzi pamoja na kondoo lililopo eneo la Kikurura wilaya ya Karagwe.

Akiwa kiwandani hapo, Dk Bashiru amepongeza jitihada za mwekezaji mzawa wa Kahama Fresh Limited, Jossam Ntangeki kwa kusaidia Kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na dira Serikali ya Awamu ya Tano katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema kiwanda hicho pia kitatoa fursa za ajira na hadi sasa kampuni hiyo imetoa ajira 130 kwa vijana wa kitanzania na kiwanda kitakapoanza uzalishaji kitatoa ajira zaidi ya 200.



Aidha Dk Bashiru kiwandani hapo alielezwa changamoto anazozipata mwekezaji ikiwa ni pamoja na kukatika umeme kila mara na kusababisha baadhi ya kazi kukwama.

Dk Bashiru alimtoa hofu mwekezaji na akawasiliana na Waziri wa Nishati Dk Medard Kalemani ili kutatua tatizo la kukatika kwa umeme katika eneo la ujenzi wa kiwanda na kuleta umeme katika eneo la ufugaji.

Dk Kalemani alimhakikishia mwekezaji kuwa changamoto hizo zitamalizwa mara moja na pia atafika eneo la uwekezaji Februari 05 mwaka huu.

Kahama Fresh Limited, kitakuwa na uwezo wa kusindika lita 10,000 za maziwa kwa siku ambapo lita 5,000 zitazalishwa na mashamba ya ufugaji ya Kahama Fresh Ltd na lita 5,000 zitazalishwa na wafugaji walioko maeneo jirani na uwekezaji huo unategemea kukamilika Juni mwaka huu.

da

wanapata elimu ya kutosha.

nane.

06/01/2021, Majira UK. 7

Cha
Ally
wa
na
cha
wa
we
na
uzi
ani

da
na
eki
ya
ya
va
po
pa
nia
aji

kt.
to
zo
a,
uzi
na
ia
u
ka
bo
ia

a
u
ti,
ia
a
ta



**Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Bashiru Ally (wa tatu kutoka kulia) akiwa ameambatana na Mkurugenzi wa Kampuni ya Kahama Fresh Limited, Jossam Ntangeki na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Karagwe, wakikagua moja ya zizi la mashamba ya ufugaji ambapo itapatikana malighafi ya kuendesha kiwanda kinachojegwa na Kampuni ya Kahama Fresh Ltd, shamaba hilo la ufugaji lipo Kikurula Kata Kihanga wilayani Karagwe mkoani Kagera juzi.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner